

Shule ya Kati ya Winburn
Kanuni ya Uhusikaji wa Wazazi na Jamii wa Title I
2019-2020
Mission Statement

Winburn Middle School, ikifanya kazi kwa ushirika na wanafunzi wetu, jamii, na jumuiya, itahakikisha kuwa kila mwanafunzi atakuwa na ujuzi wa kujenga msingi wa nguvu wa maisha kwa jumla na kimasomo ili kumwezesha kupanda ngazi kwa fanaka kuingia shule ya upili na kama mwanachama wa jumuiya anayewajibika.

Uhusiano wa karibu baina ya shule na nyumbani ni muhimu kuhakikisha na kutekeleza mfumo wa masomo wa hali ya juu kwa wanafunzi wote wa Shule ya Kati ya Winburn. Ushirika ambao unawawezesha wazazi kuhusika kwa dhati katika elimu ya watoto wao ni muhimu ili kuchangia fanaka yao ya kimasomo. Shule ya Kati ya Winburn imeazimia kuwezesha mazingara ambapo wazazi wanajua kuwa wanahitajika na Maoni yao yanakaribishwa.

Wazazi na wafanyakazi wa Winburn walishirikiana kuunda Kanuni ya Uhusikaji wa Wazazi wa Winburn. Kanuni ya Uhusikaji wa Wazazi ya 2019-2020 itaezekwa ofisini ya Shule ya Kati ya Winburn, katika ukurasa wa shule mtandaoni, ndani ya vitabu vya ajenda vya wanafunzi na itatumwa kwa posta nyumbani pamoja na ripoti za matokeo na katikati ya mhula.

Winburn itawezesha mambo yafuatayo kwa sababu ya kuhakikisha ushirika wa nguvu baina ya shule na nyumbani:

1. Ujifahamishaji wa kila mwaka ambapo wazazi watafahamishwa kuhusu mpango wa Shule Nzima wa Title I pamoja na mahitaji ya mpango wa Title I.
2. Title I Lead itafanya mikutano miwili kila mwaka wa shule, kwa ushirika wa kamati ya SBDM. Wazazi watachangia mipango, ukaguzi na uimarishaji wa mpango wa Title I kwa jumla pamoja na Kanuni ya Uhusikaji wa Wazazi.
3. Mikutano ya Uhusikaji wa Wazazi katika mwaka mzima wa shule. Mikutano ya wazazi itaangazia matokeo ya wanafunzi, mitihani ya kimasomo, mtaala wa wanafunzi, na vipimo vitakavyowawezesha wanafunzi wetu kutimia ufasaha. Warsha za wazazi, zitaangazia husiano za Wazazi/Waalimu, na ujuzi wa kusoma na kuandika. Mikutano ya ziada itakuwepo wazazi wakihitaji na itafanyika katika nyakati tofauti ili kukidhi haja za wazazi.
4. Jarida litasambazwa bila kuchelewa na litahusisha haya mambo: maelezo muhimu kuhusu mpango wa Title I, mikutano ya wazazi inayokuja na tarehe za mikutano ya wazazi/wanafunzi.
5. Wafanyakazi wa shule watatoa nafasi za angalau mikutano miwili kila mwaka wa shule baina ya wazazi na waalimu. Kuruhusu mawasiliano ya wazi kuhusu maendeleo na matokeo ya wanafunzi pamoja na habari ingine yoyote muhimu.
6. Wafanyakazi wa Shule na wazazi wataunda Kikundi cha Masomo cha Wazazi-Shule (Parent-School Learning Compact). Hiki Kikundi kitaeleza jukumu za wanafunzi, wazazi, na wafanyakazi wa shule ili kuchangia mazingara bora ya shule na matokeo mema ya wanafunzi.
7. Ukaguzi wa mwaka ambapo wazazi wote watatoa Maoni, mapendekezo ama mada zozote kuhusu mpango wa Title I. huu ukaguzi utatuwezesha kukidhi kaja za wazazi kwa njia bora.

Shule ya Kati ya Winburn itafanya kila juhudi kuwasilisha habari yoyote kuhusu mipango inayowahusu wazazi na shule, mikutano na shughuli zingine kwa lugha na mipangilio ambayo wazazi wataelewa.

Kwa sababu za kuzidisha uhusikaji wa wazazi, Shule ya Kati ya Winburn inaweza kutumia fedha za Title I kulipia gharama zozote za maana zinazohusiana na shughuli za uhusikaji wa wazazi. Hizi gharama ni kama usafiri, matembezi ya nyumbani na kutafsiri.

Kwa kutamatisha, wazazi wanakaribishwa kila wakati katika Shule ya Kati ya Winburn. Ni lengo letu kuhakikisha kuwa wazazi ni sehemu muhimu katika elimu ya watoto wao. Matokeo na fanaka ya wanafunzi yanategemea uhusikaji wa wazazi, wanafunzi, na shule.